BARUA YA PILI KWA SHEIKH ‘UBAYD AL- JÂBIRĪ
Shaykh Sālim at-Twawîl (hafidhahullāh)

5 December, 2014 | Posted by Salafibayaan | Clarifications | 735 views

“Suali: Ulianza lini kuona mabadiliko kutoka kwangu? Ikiwa ulikuwa ukijua yakwamba mimi nilikuwa kwenye daraja za mwanzo za upotofu, basi kwanini hukunipa naswiha? Naapa kwa yule ambaye Aliyeimiliki roho yangu, mimi hata sikumbuki kuwa ati ulinipa naswaha, hata sijaonana na wewe kwa muda wa miaka ya hivi karibuni na wala hapajakuwa na mawasiliano yoyote baina yetu! Kwani si katika yaliyo miongoni mwa haki yangu juu yako yakwamba unipe naswiha kabla hujanifukuza kutoka katika Sunnah?”

Kila sifa njema zinamstahiki Allâh, hapana uadui isipokuwa kwa aliye dhâlim, na mwisho mwema ni kwa wacha Mungu; twaomba swala na salamu zimshukie Mtume wetu, na juu ya jamii yake na maswahaba zake wote, amma ba’d:

Hii ni barua ya pili ninayoituma kwa Sheikh ‘Ubayd al-Jâbirî, Allâh amkirimu kwenye makaazi mawili kwa fadhla Zake zisokifani. Naituma barua hii kutokana na sababu tatu:

Ya Kwanza: Kwa vile baadhi ya maneno mapya yanayonihusu mimi yametokana na Sheikh, Allâh amuafikie kwa kila kheri.

Ya Pili: Maneno yake, Allâh Amsamehe pamoja na wazazi wake, hayakuwasilishwa kwangu makhsusi wala moja kwa moja, bali yalisambazwa katika kila pembe.
Ya Tatu: Baadhi ya ndugu fulani, Allâh Awaongoze, hawajakoma kunichafulia jina langu kwani bado wao wanajipinda katika kusababisha shaka isiyokuwa na mipaka na wakatafuta usaidizi kutoka kwa ndugu mmoja kutoka Yemen aitwae ‘Ādil Mansūr al-Bāshā, na kisha kutoka kwa ndugu mwengine wa Egypt aitwae Khālid ‘AbdurRahmān, na mwengine tena kutoka Egypt aitwae Hani’, M-Saudi mwengine aitwae Ahmad Bāzmūl, na kisha Sheikh Muhammad bin Hādī, na hatimae wote hao wakatafuta usaidizi kutoka kwa Sheikh ‘Ubayd al-Jābirī, Allâh Amuhifadhi. Kwa uwezo wa Allâh, hawatoweza kumdhuru yoyote isipokuwa watajidhuru nafsi zao wenyewe. Kwa ajili hiyo, mimi nikaonelea ni jambo la sawa niandike barua hii na niisambaze nikitarajia kutoka kwa Allâh (سبحانه وتعالى) aniruzuku Ikhlâs na usawa, na aifanye ni yenye kuwafaidisha yoyote alompangia kufaidika nayo miongoni mwa waja Wake.

Maandiko ya barua yenyewe ni kama yafuatayo:

Kutoka kwa Sālim bin Sa’d at-Twawîl, Imfikie Muheshimiwa Sheikh ‘Ubayd bin ’Abdullāh al-Jābirī, Allāh Amuhifadhi.

As-salāmu alaykum wa rahmatullāi wa barakātuhu,

Amma ba’d:

Barua yako imenifikia, Rehma za Allâh ziwe juu yako, na ni kama ifuatayo:

Muulizaji auliza: Namuomba Allâh akuonyeshe uzuri, [iwapo] mtu atasema: “Mimi naonelea yakwamba miongoni mwa wale ambao walionasibishwa na kundi la “Jam’iyyat Ihyā Turāth” kuwa ni watu wenye fadhla, ‘ilmu na U-Dini, hivi ndivyo ninavyowaona mimi na Allâh atakwenda kuwauliza na mimi simsifu yoyote kumzidi Allâh. Wao wana watu wa Qur’ân kama vile fulani na fulani...” na akawataja baadhi yao, maoni yako kuhusu maneno haya ni yapi? BārakAllāhu feekum.”

Jawabu [kutoka kwa Sheikh ‘Ubayd al-Jābirī]:

“Mtu mwenye kuyasema maneno haya ni mbishi na hili ni katika udanganyifu wa pili miongoni mwa udanganyifu utokao kwake ambao uliowasilishwa katika mjumuiko huu, wa mwisho natumai uliwasilishwa siku ya Jumapili... msingi walio nao Ahlul ‘ilm ni kwamba mwenye mafungamano na watu wazushi na asiwakanye na asiwasaidie wenye kuwakabili hao anafaa achukuliwe kuwa ni miongoni mwao. Hii ni hata kama atakua dhahiri yake anaonekana kuwa ni mtu mwema kutekeleza mambo yake kulingana na Sunnah – kwani hili halimuokoi yeye kutokamana na kutumbukia kwenye

uzushi yeye mwenyewe. Sisi tumeyazungumza kuhusu kundi la Ihya ut-Turāth kwenye vikao vingi katika nchi ya Kuwait na hapa vilevile tumewazungumza kama inavyopaswa, kwahivyo yoyote apendae anaweza kuirejelea hiyo, Jum'iyyah hiyo [Ihyā ut-Turāth] imo miongoni mwa vigawanyo vya Ikhwânul Muslimîn."

[Mwisho wa maneno ya Muheshimiwa Sheikh]

Mimi nasema, tena Naapa kwa jina la Allâh aliye Pekee, naomba msaada, na juu yake najitegemeza na kumuelekea Yeye:

Kwanza: Unahitajika ujue, Ewe muheshimiwa Sheikh 'Ubayd, Allâh akuhifadhi, yakwamba maneno yangu uliyoyaliziwa kwayo, mimi niliyaandika kitambo sana kwenye nakala na ilikuwa inamuhusu mmojawapo wa ndugu wa kutoka Ihyā ut-Turāth, ambaye aliyenituhumu mimi kwa kuwakashifu kila waliojinasibisha na Jam'iyyah zao pasi na kubagua. Kwahivyo, niliandika maneno hayo yaliyowahi kuwasilishwa kwako na hao ndugu hawakukutanabahisha uhifadhi jawabu lako isipokuwa baada ya kumzungumza ndugu Ahmad Bāzmūl! Inawezekana kuwa dhamira yao ilikuwa ni kuwaepusha watu wasikusikilize kwenye uliyokuwa ukiyasema kumuhusu ndugu Ahmad Bāzmūl, na hili haliko mbali kulingana na tajriba yangu kuwahusu wao.

Pili: Baadhi ya ndugu nchini Kuwait na sehemu nyenginezo huyaficha maneno yako kabisa kumuhusu Ahmad Bāzmūl na wala hawakuyasambaza ili wapate kumkinga mwenzao Bāzmūl ahifadhike. .

Tatu: Wanayazingatia maneno yako kumuhusu Bāzmūl kuwa ni **"fitna"** na kwamba yanapaswa kunyamaziwa na wakatoa naswaha hizo yakwamba **"itolewe amri ya kukatazwa kuingilia mas'ala hayo"** na kwamba **"mazungumzo kuhusiana na hayo yawachiwe ma-'Ulamâ'"!?** Na wamesema **"jishughulisheni na kutafuta 'ilmu na muwachane na kumzungumza Bāzmūl"!?** [1] Mimi sijui ni kwa nini maneno uliyoyasema kumuhusu Bāzmūl kwamba ni **"fitna"** ambayo **"inayopaswa kuwachiwa ma-'Ulamâ'** haliyakuwa maneno yako kuwahusu watu wengine husambazwa kila kipembe, yakashughulikiwa vilivyo mbali na kutafuta 'ilmu, na wala wasiachiwe ma-'Ulamâ'"?! Mimi siwajui hao ma-'Ulamâ' watakaotoa maoni juu ya neno lako? Na sijui ni lini itakapofanywa uchunguzi kuihusu hukmu yako juu yake? Na sijui ni lini itakaposambazwa hukmu ya mwisho!? SubhānAllāh, fitan ni pale mambo yanapochanganyikiwa na haki zikapuuzwa, kama alivyosema Sheikh al-'Allâmah 'Abdul'Azeez bin Bāz *(rahimahullāh)* katika *Majmū' al-Fatāwā wa'l-Maqālāt*, vol.7, Uk.363:

[1] **[Nukta ya mfasiri (wa ki-Ingereza), 'AbdulHaq]:** mfano mwengine mzuri sana wa ndumila kuwili (double-standard) na kucheza michezo na watu wenye hisiya kali za Ghuluw, ni kwamba wao wanamuhimiza kila mtu **"achukuwe msimamo"** juu ya ma-Sheikh wasioafikiyana nao wao, kisha pindi

anaposhambuliwa mmojawapo wa mashekhe zao na kukashifiwa, hata ikawa ni Sheikh mwengine ambaye wao humfuata ki-Upofu, hukataa yote hayo wakarudi nyuma kwenye msimamo wa **"musijiingize"!**? Ingawaje, zaidi ya miaka Kumi na Tatu iliyopita, wakati mzozo baina ya Ahlus –Sunnah ulipotokea, ma-'Ulamâ' kama vile Mashekhe wa Jordan, Muhaddith wa Madînah 'AbdulMuhsin al-'Abbād al-Badr, al-'Allāmah Fawzān na Shaykh 'AbdusSalām Burjis *(rahimahullāh)* walikuwa wakitoa naswiha yakwamba watu wasijishughulishe kwenye mtafaruku miongoni mwa watu wa Sunnah, watu hawa hawa waliyakataa yote hayo na badala yake wakaendelea kuzidisha fitna, wakiwalazimisha vijana wachukuwe misimamo na kupoteza wakati na mizozo kama hiyo. Mpaka sasa hivi kumewekwa rufaa ya watu wasiojulikana kwa min-ajil ya kuyakengeusha maneno ya Sheikh 'Ubayd ya kumuhusu Ahmad Bāzmūl, na wakayakanusha mas'ala hayo kabisa

Kwahiyo, kuna mchezo wa kuchagua ni kwenye mizozo ipi unafaa kuingia ukatia chumvi na ipi ambayo, ikibidi, unafagia kwa uangalifu chini ya zulia.

Naridhika kukupasha habari yakwamba, ahâdîth zinazohusiana na fitan na kutahadharishwa dhidi yake huzingatiwa na wanavyuoni kuwa ni fitna ambazo mwenye haki hawezi kutafautishwa na asiyekuwa na haki, fitna hizi wameonywa waumini wajitahadhari nazo. Nazo ndizo zile ambazo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alizokuwa amekusudia kwa maneno yake aliposema, "... na aliyekaa ni bora kuliko aliyesimama, na aliyesimama ni bora kuliko anayetembea, na anayetembea ni bora kuliko anayekimbia." Ama kuhusu fitna ambazo mwenye haki anatambulika kutokamana na asiyekuwa na haki, na dhâlim anatambulika kutokamana na aliyedhulumiwa, basi hii siyo iliyokusudiwa kwenye hadith iliyotajwa hapo juu. Bali, dalili za kisheriya kutoka katika Kitâb na Sunnah, inaashiriya uwajibu wa kumsaidia mwenye haki juu ya asiyekuwa na haki na mnyonge juu ya mwenye nguvu na dhâlim.

[Mwisho wa maneno yake, Rehma za Allâh ziwe juu yake]

Nne: Iwapo wao kweli walitaka kudumisha umoja kwa neno na wasichochee fitnah, basi wasingeliyasambaza maneno yako kuhusu Mashekhe wa Yemen na wangelijitahidi kurekebisha. Juu ya hayo, kwa bahati mbaya, wao huyataja yale yanayoafikiyana na wao na hawayataji yanayokwenda kinyume na wao.

Tano: Muheshimiwa Sheikh 'Ubayd, Allâh Akuafikiye katika kila kheri, mimi nilitaja kwenye maneno yangu yaliyotangulia kukuhusu wewe yakwamba umenijua mimi kwa takriban miaka 21, na bado tena ndani ya wiki moja umeshanizungumza mara mbili na pana uwezekano yakwamba kwenye masiku yajayo utakuja kunizungumza tena kwa maneno mapya.

Suali: "Ulianza lini kuona mabadiliko kutoka kwangu? Ikiwa ulikuwa ukijua yakwamba mimi nilikuwa kwenye daraja za mwanzoni za upotofu, basi kwanini hukunipa naswaha? Naapa kwa yule ambaye roho yangu iko kwenye mikono

Yake, mimi hata sikukumbuki ukinipa naswaha, mimi hata sijakuona kwa muda wa miaka michache, na wala hatujawahi kuwa na mawasiliano ya aina yoyote! Jee, mimi sina haki juu yako yakwamba unipe naswaha kabla hujanifukuza kutoka kwenye Sunnah ukanipachika na wengine?

Sita: Muheshimiwa Sheikh, ikiwa hali ni kwamba wewe hutaki kunipa naswaha kwa sababu yoyote maalum, basi ni kwanini, angalau kwa uchache, huyathibitishi yaliyowasilishwa kwako? Kwani si Allâh (سبحانه وتعالى) alisema kuwa:

« يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنْ جَاءَكُمْ فَاسِقٌ بِنَبَإٍ فَتَبَيَّنُوا أَنْ تُصِيبُوا قَوْمًا بِجَهَالَةٍ فَتُصْبِحُوا عَلَى مَا فَعَلْتُمْ نَادِمِينَ »

“Enyi mlioamini! Kama fasiki, (asiyekuwa wa kutegemewa) akikujieni na habari (yoyote ile msimkubalie tu) bali pelelezeni (kwanza), msije mkawadhuru watu kwa ujahili na mkawa wenye kujuta juu ya yale mliyoyatenda.”
{al-Hujurāt (49): 6}

Saba: Pindi muulizaji alipokuuliza hakukutajia majina ya Mashekhe ambao nilowasifu katika nakala yangu ya asili! Labda palikuwa na makusudio fulani katika hilo, Allâh Anajua zaidi. Kwahiyo, mimi nataka kutaja majina yao kwa lengo muhimu sana:

Nane: Mashekhe wenyewe ni: Sheikh Hamūd an-Najdī, Sheikh Dāwud al-’As’ūsī, Sheikh Faisal Qazār al-Jāsim,[1] Sheikh Ibrāheem al-Ansārī.

[1] **[Nukta ya mfasiri (wa ki-Ingereza), ’AbdulHaq]:** Sheikh Faisal alitangaza kujiepusha kwake kutoka Ihyā ut-Turāth tangu miezi Kumi na Nane iliyopita.

Tisa: Muheshimiwa Sheikh ‘Ubayd, Allâh Akupe furaha hapa ulimwenguni na kesho Akhera, jee, hao Mashekhe wanne ni “*Mubtadi’ah”* (wazushi)? Ema uwazingatie kuwa ni “*Mubtadi’ah”* ambao, iwapo itakuwa hivyo nijulishe kuhusu bid’ah zao zilizowatoa kwenye mviringo wa Ahl us-Sunnah, au wao ni miongoni mwa Ahl us-Sunnah. Kwahiyo, ni kwanini umezingatia kuwasifu kwangu kuwa ni “urongo (mmoja) unaotokamana na urongo (mwingi)”? Haifichiki kutoka kwako yakwamba hakuna matatizo kulingana na Sheriya ya Uislamu, akili na desturi katika kumsifu kama anavyostahili Muislamu aliye Sunni tena *Muwahhid*.

Kumi: Mimi sijawahi maishani mwangu kusema yakwamba hao Mashekhe waliotajwa hapo juu ni wazushi, na wala sitobadilisha maoni yangu kuwahusu wao. Kwahiyo, sijawahi kuwa na rai ya awali kuwahusu wao kisha rai ya baadae, au maoni ya zamani na kisha maoni mapya. Rai yangu kuwahusu wao kwa kiyasi cha robo qarne, au zaidi au hata kwa uchache, imekuwa yakwamba wao ni Ndugu, Waislamu walio Muwahhidin, wao si Mitume na wala si

watakatifu. Mimi nakataa kutoka kwao linalonidhihirikia kwangu kuwa ni kosa, na mimi nawanaswihi na pia kuwakosoa, nao wananipa mimi naswaha na kunikosoa na wala sijitweki wao katika nafsi yangu.

Kumi na Moja: Mimi sijawahi maishani mwangu kumsikiya Sheikh yoyote akiwafanyia *tabdi'* hao Mashekhe nilowataja hapo juu. Hata ndugu Muhammad al-'Anjarī, Ahmad Bāzmūl, Ahmad Subay'ī, Fawwāz al-'Awdī, Zayd bin Hulays, Tāriq bin Husayn, Khālid 'AbdurRahmān al-Misrī – hao wote hawawafanyii *tabdi'* Mashekhe wa Jam'iyyah Ihyāt Turāth, kulingana na nijuavyo mimi, isipokuwa iwapo watafanya *tabdi'* kwa njia ya siri na Allâh anaijua siri, na pana uwezekano kwako wewe, Muheshimiwa Sheikh kuwauliza na kuthibitisha kutoka kwao wewe mwenyewe.

Kumi na Mbili: Muheshimiwa Sheikh, haikufichika kwako yakwamba *Tabdi'* ya Muislamu na kumtoa kutoka kwenye Sunnah si jambo sahali. Uzushi ni Qarînah ya Shirk na ni jambo ovu mno, kila la uzushi ni upotofu, na kila aina ya upotofu utamalizikia motoni, kwahiyo, matamshi yako, Muheshimiwa Sheikh yakwamba: "... misingi ya Ahl us-Sunnah ni kwamba mwenye kushirikiana na watu wazushi na asiwaonye kuhusiana na uzushi wao na asiwasaidie wale wenye kuwakabili anapaswa kuzingatiwa naye kwamba yuko pamoja nao. Haya ni, ingawaje huwenda akawa dhahiri yake yeye ni mtu mwema na akatekeleza kulingana na Sunnah – kwani hili halimuokoi yeye kutokamana na kutumbukia kwenye uzushi yeye mwenyewe."

Mimi nasema: Imefahamika kutokamana na maneno yako, Muheshimiwa Sheikh, na mimi natumai yakwamba nimekosea katika ufahamu wangu, yakwamba wewe umewafanyia *tabdi'* hao Mashekhe pamoja na mimi vilevile! Hili ni suala la hatari kubwa, kama alivyosema Imâm Ahmad: "Kuwatoa watu kutoka katika Sunnah ni jambo zito sana", kama ilivyosimuliwa na al-Khallāl katika *as-Sunnah*, vol.2, Uk.373, no.513. Kwa hakika, hata kama husemwa kuhusu haki za Muislamu: "Ewe Fâjir, ewe Fâsiq" ni sahali kuliko kumwita: "Ewe mzushi, ewe mpotofu."

Kumi na Tatu: Muheshimiwa Sheikh 'Ubayd, kufikia kwenye nukta hii, nitakusimulia wewe maneno ya Imām wa Ahl us-Sunnah, baba yao ma'Ulamâ' na wanafunzi wa ki-'ilimu, mwalimu wa kihakika na baba mkarimu ambaye ummah ulimpoteza na tangu baada ya kuondoka yeye ugeni ukazidi, muheshimiwa Sheikh 'Abdul'Azeez bin 'Abdullāh bin Bāz *(rahimahullāh)*. Alisema: "Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) amesema: *'Watoto wote wa Adam hufanya makosa, na mbora wa wale wenye kukosea ni wale wenye kutubia'*. Vilevile, maneno ya ma-'Ulamâ', Mâlik (رحمه الله) amesema: 'Hakuna yoyote miongoni mwetu sisi ambaye maneno yake yanaweza kukubaliwa au kukataliwa, isipokuwa maneno ya mwenye kaburi hili.' [akiashiriya kaburi la Mtume (صلى الله عليه وسلم)]. Kila mwanachuoni hakosi makosa, kwahivyo ni wajibu kumtanabahisha kuhusiana na makosa yake kwa njia nzuri. Hata hivyo, hafai kutahadharishwa kwa watu awapo ni miongoni mwa Ahlus Sunnah, bali anafaa

aonyeshwe uongofu kunako wema na afunzwe yaliyo mazuri, na anasihiwe kwa njia ya rifq katika ulinganizi wake kwa Allâh (سبحانه وتعالى), na atanabahishwe kuhusiana na makosa yake. Watu walinganiwe wakafaidike kwa ilmu kutoka kwake, na waongeze ufahamu kutoka kwake maadamu atakuwa ni wa Ahl us-Sunnah wal Jamâ'ah.

Na makosa hayalazimishi yakwamba watu watahadharishwe naye, lakini hata hivyo linafaa libainishwe kwani kila mtu ni mwenye kufanya makosa, hili ni pamoja na kuzingatia yaliyo mazuri kutoka kwake na anayojulikana nayo kutokamana na aqida nzuri. Kwahiyo, ni wajibu juu ya walinganizi kwenye njia ya Allâh, wawe na busara, wawe wapole, wasiwe na pupa katika hali zao, waijue haki, asiwe ametahadharishwa na wanavyuoni na awe na tahadhari dhidi ya njia za uadui na chuki. Bali, wanahitajika wadumishe njia zote za umoja miongoni mwa Ahlul 'ilm na Ahl us-Sunnah wa'l-Jama'ah katika da'wah yao katika njia ya Allâh na ulinganizi wao kwa watu katika yaliyo mazuri. Hili ni kwa ajili ya walinganizi katika njia ya Allâh waongezeke kila mahali ili da'wah iwafikie watu. Iwapo watu watakuwa ni wenye kusikiya yakwamba hawa wanawatahadharisha wale na wale wanawatahadharisha hawa, basi wanatatizika, da'wah inapotea muelekeo wake na watu wanabakia na dhana mbaya kuihusu da'wah."

Mwisho wa maneno yake, rehma za Allâh ziwe juu yake.

Kutokana na mawaidha yaliyotolewa na muheshimiwa Sheikh katika mojawapo ya "Jam'iyyat ul-Khariyyah in Kuwait" kwa njia ya simu, tarehe 10/10/1416, na inaweza kupatikana kwenye mtandao rasmi wa Sheikh. Lau kama ungelikuwa ni mwenye kuyalinganisha maneno yako, muheshimiwa Sheikh ['Ubayd] kuwahusu Ahl us-Sunnah kwa uongofu wa Shaykh al-'Allāmah 'Abdul'Azeez bin 'Abdullāh bin Bāz (رحمه الله)

Kumi na Nne: Wanavyuoni wanaweza kukhitilafiana kumuhusu mtu, baadhi yao wanaweza kumfanyia *tabdi'* na wengine wasimfanyie, na wala sio kwamba hawamfanyii *tabdi'* tu, bali wanamsifu na kumtukuza haswa. Kwahivyo sio sharuti kuwaambatisha wote ambao wasomfanyia *tabdi'* yoyote ambaye unaemuona kuwa ni mzuri kwake na kumzingatia yeye kuwa ni mzushi kama yeye. Lau kama tungelifanya hivyo, basi tutaingia kwenye mfululizo wa *tabdi'* ili maneno yangu yaeleweke vizuri, nitakuletea mfano ule wa Sheikh Bakr Abū Zayd*(rahimahullāh)*.

"Ewe muheshimiwa Sheikh ['Ubayd], mfanyie *tabdi'* kama inavyofahamika, uliposema kumuhusu yeye: "Ikhwānī Qutbī anayeteketea, asiyestahiki kusifiwa."
Labda ulikusudia kwa jina hilo "Qutbī", mzushi, kisha jee akiwa "anateketea"?! Ikiwa ufahamu wangu ni wa makosa, basi naomba msamaha wa Allâh na natubia Kwake Yeye. Wanavyuoni wengine wamemsifu Sheikh Bakr Abū Zayd, na kama ilivyo wazi, yeye alikuwa ni miongoni mwa Wanavyuoni wakubwa wa Jumuiya

rasmi, akawekwa kwenye cheo na kiongozi kwa ushauri wa wanavyuoni wakubwa. Miongoni mwa waliomsifu ni: sheikh wetu Ibn 'Uthaymeen *(rahimahullāh);* aliyesema kumuhusu yeye:

"Ndugu yetu, Sheikh Bakr Abū Zayd ni miongoni mwa Wanavyuoni wakubwa, na ni maarufu sana kwa kutoa uamuzi na muangalifu katika mas'ala kwa undani... kwa vile amewahi kushikilia nyadhifa mbalimbali, na vitendo vyake vyote viliashiriya yakwamba alikuwa anafaa kuwa katika kushikilia nafasi hizo. Sasa yuko kwenye Lajnah ya Fatāwā inayo ongozwa na muheshimiwa Sheikh 'Abdul'Azeez bin Bāz katika mji wa Riyâdh na pamoja na Baraza la Wanavyuoni Wakubwa. Twamuomba Allâh atuafikie sisi pamoja na yeye. Zaidi ya hayo, mafungamano baina ya lugha yake na uandishi aliokuwa nao inaashiriya umahiri wake kwenye lugha ya kiarabu na kwahivyo wakati mwengine makamusi huhitajika kufahamisha istilahi anazotumia. Juu ya yote hayo, hapakuwa na uzito wowote kwake. Hii yaonyesha yakwamba Allâh alimruzuku ukundufu mkubwa wa asili kwenye lugha ya kiarabu, wakati ambapo ma'Ulamaa wengi waliokuwa katika zama zake hawakuweza kushika hayo kiyasi cha kwamba hata utakuja kusema yakwamba milango hii ni mfano wa Maqāmāh ya al-Harīrī, ambayo ni maarufu kwa wengi wenu yakuwa ni Maqāmat nzuri yenye mawaidha na maneno mengi ambayo mtu anaweza kufaidika kutokamana nayo.

Mwisho wa maneno ya Sheikh Ibn 'Uthaymîn kutoka katika utangulizi wa *Hilyat Tālib ul-'Ilm*.

Kumi na Tano: Haikufichika kutoka kwako, muheshimiwa Sheikh 'Ubayd yakwamba Sheikh Rabī' bin Hādī al-Madkhalī, Allâh Amuhifadhi, alimkosoa Sheikh Bakr Abū Zayd *(rahimahullāh)*, kwa njia ya utaalamu na majibu yenye manufaa ambayo yaliyochapishwa na kutolewa. Juu ya yote hayo, alitamka maneno yake mashuhuri yakwamba hamfanyii *tabdi'* Sheikh Bakr Abū Zayd! Sheikh 'Ubayd, lau kama ungelimfikiria kijana wa ki-Islamu anayesikia hukmu hizi na maneno yenye uzito, kutokamana na mengi uliyoyasema kuwahusu wanavyuoni, kama vile, "mpotofu, takataka, mzushi, Ikhwānī, Qutbī, mughaafala, na mfano wake." Haliyakuwa kuna ma-'Ulamaa wengine waliowasifu, walikuwa na fikra nzuri juu yao, wanaswihi wanafunzi wa ki-ilimu wafaidike kutoka kwao. Mimi nasema, ewe muheshimiwa Sheikh, yatakikana utaamali juu ya wanafunzi wadogo wa ki-ilimu na ambao asili yao si waarabu, na yatakayowasibu wakiwa baina yao, pindi watakaposikiya mfarakano huu baina ya ma-'Ulamaa.

Kumi Na Sita: vilevile, Sheikh al-'Allāmah, Sālih bin Fawzān al-Fawzān, Allāh Amuhifadhi, aliwapa naswaha baadhi ya wanafunzi wa ki-ilimu, ambapo aliwaonya kutokamana nna kusema "fulani na fulani si ma-Salafi" na maneno yake ni mashuhuri katika mas'ala haya pindi alipoulizwa:

"Hivi karibuni, kumeibuka mambo ya kubandikana majina kwa kupitia misemo kama "fulani na fulani si ma-Salafi" na "fulani na fulani si miongoni mwa ma-

Salafi" – sasa nauliza, "misemo kama hiyo inazingatiwa kuwa tabdi'? Na inahitajika kupatikana dalili juu yake?"

Jawabu kutoka kwa al-'Allāmah Sālih al-Fawzān:

Wallâhi, mimi nilitoa onyo kutokamana na kubandikana majina kama hayo, kila sifa njema zinamstahiki Allâh. Vijana wa ki-Islamu na wanafunzi wa ki-ilimu , kwa uwezo wa Allâh, wote wako juu ya wema na juu ya aqida ya Salaf, hata kama miongoni mwa baadhi yao kunapatikana upungufu na ujinga, jambo hili haliwafukuzi wao kutoka katika Salafiyyah. Maneno haya hayaruhusiwi, maneno haya hayaruhusiwi miongoni mwa ndugu moja, wanafunzi wa ki-ilimu na watoto wa Waislamu kwenye miji ya Waislamu. Maneno haya hayaruhusiwi. Panatakiwa kupatikane kupeana naswaha, ukimchunguza ndugu yako mwenye mambo hayo, mpe naswiha. Ama kwako wewe kumbwaga daraja yake kwa kupitia kwenye majina, ukamwambia yakwamba yeye hako kwenye njia ya Salaf, na hayuko kwenye Salafiyyah, basi labda wewe mwenyewe hujui maana ya Salafiyyah. Juu ya hayo, kama wanavyodai baadhi yao U-salafiyyah, na kumbe hawaujui ni nini... lau utamuuliza kuhusu Salafiyyah, na ni nini hatojua.

Mwisho wa maneno yake.

Kumi na Saba: Muheshimiwa Sheikh 'Ubayd, Allâh Akuhifadhi, Ulimwengu wa ki-Islamu umezalisha ma-Imâm Mashuhuri ambao Ahl us-Sunnah hawakukhitilafiana juu yao, kama vile Sheikh al-'Allāmah 'Abdul'Azeez bin Bāz, Sheikh al-'Allāmah Muhammad Nāsiruddeen al-Albānī, Sheikh al-'Allāmah Muhammad bin Sālih al-'Uthaymeen na Sheikh al-'Allāmah Muqbil bin Hādī al-Wādi'ī, Allâh Awahifadhi wote hao – na kulingana na orodha yako, hakuna mwanachuoni [muaminifu] aliyetokeza kutoka kwenye wanavyuoni hao, au baadhi yao, isipokuwa kwa idadi iwezekanayo kuhesabika kwa mkono mmoja tu!?

Kumi na Nane: Inapaswa ujuwe, muheshimiwa Sheikh yakwamba baadhi ya wale wanaosambaza maneno yako yakwamba Baraza la wanavyuoni Wakubwa limekusanya ma- Qutbī na wazushi, na hapana shaka yoyote yakwamba maneno haya yanaitweza Baraza na yakawafanya watu wawe na shaka nalo, kama alivyosema Sheikh wetu Ibn 'Uthaymeen *(rahimahullāh)*.

Muheshimiwa Sheikh mimi bado sijamaliza kukuandikia barua zangu, kwani nitakuandikia ya tatu Allâh Akipenda.

Killa sifa njema inamstahiki Allâh, mwanzo na mwisho,kwa dhahiri na kwa siri, na twamuombea swala, salamu na baraka zimshukie Mtume Muhammad, jamii yake na Maswahaba zake wote.

Shaykh Sālim at-Taweel, *Wa Aydhan Risālah Lam Yahmiluhā al-Bareed ilā Fadeelat ish-Shaykh 'Ubayd bin Hādī al-Jābirī hafidhahu Allāh, 2-3*. [Na pia, barua isiyoweza kutumwa kwa Posta kwa Sheikh 'Ubayd al-Jābirī, Allâh Amuhifadhi, Barua ya 2nd katika barua 3]. Tarehe 24 Muharram 1436 AH/17 November 2014 CE,Tizama:

http://www.saltaweel.com/articles/372

Tafsiri kwa mukhtasari: 'AbdulHaq al-Ashanti

Tafsiri kwa Kiswahili: Abu Farida Muhammad Basawad

The Qur'an And Sunnah Society od East Africa. [QSSEA]

Mombasa, Kenya